HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI

SHULE YA SEKONDARI ITIGI

Mkuu wa shule +**255 756 658 415**
M/Mkuu wa shule +**255 762 624 935**
Patron **+255 759 394 420**

S.L.P. 10,
ITIGI.

Kumb. Na ***ITG/SS/KJ/KDT V/2022*** Tarehe 29/03/2022.

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …….
S.L.P ……
……

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ITIGI HALMSHAURI YA ITIGI MKOA SINGIDA MWAKA 2022**

1.0 **UTANGULIZI:**

Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano mwaka wa masomo 2022/2023 katika shule hii kwa tahasusi ya **HGL/HGK**

Shule ipo Mkoa wa Singida Halmashauri ya Itigi, ipo umbali wa Kilomita 1 (moja) kutoka makao makuu ya mji wa Itigi. Waweza kufika shuleni kwa usafiri wa reli ya kati au basi.

Muhula wa masomo unaanza tarehe**……** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **…….** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **……** saa 12: 00 jioni.

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia**: -

2.1 **Sare ya Shule**

(a) Sare ya shule ni suruali **2** rangi ya **dark blue** kitambaa **suit material (estim)** Suruali iwe na **tanapu chini**, **linda 2** na chini iwe na upana wa sentimeta 16 (mzunguko 32 cm isiwe modal au chupa ya kubana)
(b) Shati **2** rangi nyeupe mikono mirefu
(c) Tai ya dark blue yenye strips (mistari) nyeupe (inapatikana shuleni aje na Tsh. 5,000/=)
(d) Viatu vya shule ni rangi **nyeusi** vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
(e) Soksi jozi mbili (2) nyeupe
(f) Sweta rangi ya dark blue shingo ya “V” (linapatikana shuleni aje na Tsh. 15,000/=)
(g) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa **ngozi** usio na mapambo
(h) Nguo za kushindia (shamba dress) suruali yenye rangi ya **kaki** kitambaa **suit material**
(i) Sare ya michezo ni jezi nyekundu (**isiyo na maandishi wala nembo yoyote**) na bukta ya bluu
(j) T-shirt rangi ya **dark blue** inapatikana shuleni kwa Tshs. 15,000/= (Njoo na Fedha)
(k) Viatu vya michezo ni vya rangi yoyote

TANBIHI: Hairuhusiwi mwanafunzi kuja na nguo za nyumbani.

2.2 Ada na Michango ya Shule

a) Ada ya shule kwa mwaka ni Tshs. 70,000/=, unaweza kulipa yote au kwa muhula Tshs. 35,000/=

b) **Michango Mingine inayolipwa na mwanafunzi kwa mwaka ni:-**

i. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
ii. Shilingi 35,000/= kwa ajili ya wapishi, walinzi na vibarua wengine
iii. Shilingi 5,000/= kwa ajili ya kitambulisho
iv. Shilingi 18,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
v. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza Tshs 5000/= Bima ya afya na Tshs.5000/= tahadhari usafiri na n.k (Wanafunzi wenye Bima za Afya waje na kadi za Bima ya Afya na shilingi 5000/= ya tahadhari kama usafiri na n.k)
NB. Mzazi/mlezi unashauriwa kumkatia mwanao bima kubwa ya NHIF kwa ajili ya matibabu. Endapo mwanafunzi atatibiwa au kulazwa katika hospitali binafsi, mzazi atahusika na gharama zote za matibabu
vi. Shilingi 25,000/= mitihani ya kujipima
vii. Shilingi 5000/= kwa ajili ya tahadhari (haitarejeshwa)
<u>Jumla ya MICHANGO MINGINE</u> ni Tshs. 118,000/=

***<u>ANGALIZO</u>*:**

- Jumla ya **ADA** na **MICHANGO MINGINE** kwa mwaka ni **TSHS. 188,000/=**

- **Hakikisha Pay in slip ziwe mbili (2) tu**, Moja ya **ADA** tu na nyingine ya **MICHANGO MINGINE** (**usichanganye ada na michango mingine kwenye pay in slip moja**) na fedha zote ziwekwe katika benki ya NMB Akaunti Na. ***50701100052* – ITIGI SECONDARY SCHOOL RECCURENT.** Aidha mwanafunzi aje na Pay in slip 2 alizolipia na ziwe zimeandikwa jina la mwanafunzi siyo la mtu mwingine, **Mfano Samwel Ally Mbogo- kidato cha Tano** (fedha tasilimu hazipokelewi)

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni: -

(i) Ream 2 ya karatasi aina ya **A4** kwa mwaka
(ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (HGL/HGK)
(iii) Scientific calculator
(iv) Godoro (2½ kwa 6) aje nalo
(v) Mashuka pair 2 rangi ya bluu bahari, blanket 1, foronya 1 na Chandarua 1 (2½ kwa 6)
(vi) Vyombo vya chakula ambavyo ni sahani, bakuli, kijiko na kikombe (vya aluminium, vya plastic havipokelewi)
(vii) Ndoo 2 ndogo zenye mifuniko (ujazo wa lita kumi)
(viii) Squizer 1, Jembe jipya na mpini wake 1, Shoka 1, Mfagio mgumu na laini 1 (soft na hard brooms), Mfagio wa nje 1 (chelewa) na panga 1,
(ix) Dawa ya kusafishia choo (aina careline) lita tano (5) kwa ajili ya usafi
(x) Picha nne (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa Mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu. (lazima aje nazo)
(xi) Galoni la ujazo wa Lita tano (5) kwaajili ya kuhifadhia maji ya kunywa

NB:

(a) Mwanafunzi aje na Nakala (copy) ya CHETI CHA MATOKEO (**RESULT SLIP**) cha kidato cha nne na cheti cha kuzaliwa kwa ajili ya utambulisho wake

(b) Fomu namba Nne (4) na namba Tano (5) ziwasilishwe ofisi ya makamu mkuu wa shule zikiwa zimejazwa kikamilifu na kusainiwa

(c) Mzazi unashauriwa kumfungulia mwanao akaunti ya Benki ya NMB au CRDB ili kuepuka usumbufu

(d) **Epuka matapeli wanaopiga simu kwa wazazi kuwaomba fedha au kutoa taarifa ya ugonjwa, mawasiliano yote yafanyike kupitia namba za simu zilizopo katika fomu hii tu na si vinginevyo.**

3.0 SHERIA MUHIMU ZA SHULE NA MAKOSA YATAKAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI

a) Wizi.
b) Uasherati, ubakaji, ushoga, ulawiti na usagaji.
c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, biashara ya madawa ya kulevya.
d) Makosa mengine ya jinai.
e) Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake au mtumishi.
f) Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine.
g) Kudharau bendera ya taifa, picha za viongozi wa taifa, nembo ya taifa, wimbo wa taifa na fedha za taifa.
h) Kuoa au kuolewa.
i) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
j) Kutoa au kushawishi kutoa mimba.
k) Kugoma, kufanya fujo, kushawishi, kuchochea na kuongoza migomo, au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni, kutoa lugha ya matusi kwa kiongozi wako au kwa mwanafunzi mwenzako.
l) Kukataa adhabu halali.
m) Kujiachisha shule mwenyewe.
n) Kumiliki au kutumia simu ndani ya eneo la shule ambapo simu ikikamatwa itataifishwa na utafukuzwa shule mara moja. (**mwanafunzi asije na simu shuleni**)
o) Kuchelewa kufika shuleni kwa muda halali uliopendekezwa na shule
p) Ni marufuku kutembelea nyumba za walimu bila ruhusa maalumu
q) Kutokuvaa sare elekezi ya shule, mfano viatu, sketi, suruali, Tisheti n.k
r) Kufuga ndevu, kusuka, au kuachia nywele ndefu kichwani.
s) Kuwa nje ya darasa wakati wa vipindi.
t) Kumgomea kiongozi halali aliyeteuliwa au kuthibitishwa na serikali kuu au Baraza la serikali ya wanafunzi kwa ajili ya kuongoza.
u) Ni marufuku kuwa ndani ya eneo la shule baada ya saa 12:00 jioni (kwa wanafunzi wa kutwa) na unatakiwa kuwa ndani ya eneo la shule kabla ya saa 12:00 jioni (kwa wanafunzi wa Bweni)
v) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama sumu n.k

AIDHA

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayanzi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kuripoti shuleni:

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
(e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
(f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
(h) Kutunza mali za Umma

N:B Wanafunzi hawaruhusiwi :

i. Kuja na simu shululeni wakati wowote
ii. Kusuka, kunyoa mitindo wala kufuga ndevu

4.0. Mambo mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na Mwanafunzi:

i. Medical Examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali, (Na Sio Zahanati au Kituo cha Afya binafsi) na itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
ii. Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na Sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule.

Karibu Sana Shule ya Sekondari Itigi

Jacob P. Mwabeza

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI ITIGI
S.L.P. 10
ITIGI

Nakala: Katibu Mkuu
Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi,
S.L.P 9121,
DAR ES SALAAM.

Katibu Mkuu,
TAMISEMI,
S.L.P 9123,
DODOMA.

Afisa Elimu Sekondari (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Itigi,
S.L.P 70,
ITIGI.

Simu: Mkuu wa Shule 0756 658 415/ 0673 988 415 S.L.P. 10,

Makamu M/Shule 0762 624 935/0735 627 770 **ITIGI**

Picha ya Mwanafunzi

A. FOMU YA MKATABA NA MWANAFUNZI

MIMI …….

WA S.L.P …….

Naikubali nafasi hii ya kidato cha TANO tahasusi ya HGL/HGK niliyopewa katika shule hii, na nakubali kutii Sheria zote za Shule zilizopo na zile zote zitakazotolewa kwa muda wowote. Aidha ninaahidi kutoshiriki mgomo, fujo na makosa ya jinai. Naahidi kutomiliki wala kutumia simu ya mkononi mazingira ya shule bila idhini. Ninaahidi kuwatii Walimu, Wafanyakazi wasio walimu na Viongozi wa Serikali ya wanafunzi watakaochaguliwa kwa mujibu wa Sheria.

Ninaahidi kuwa mwaminifu na kuwa nitajielimisha kwa kadiri ya uwezo wangu wote kwa manufaa yangu na Taifa lote kwa ujumla

SAINI YA MWANAFUNZI ……

B. FOMU YA MKATABA NA MZAZI/ MLEZI

MIMI …….

WA S.L.P …….

Ninakubaliana na sheria/ kanuni zilizowekwa na kuambatanishwa kwenye fomu ya kujiunga na shule. Nitakubaliana na adhabu itakayotolewa na Uongozi wa shule ikiwa mwanangu atavunja/atakiuka sheria hizo.

Picha ya Mzazi/Mlezi

SAINI YA MZAZI / MLEZI …….
NAMBA YA SIMU …….
TAREHE …….....

C. SEHEMU HII IJAZWE NA MTENDAJI WA KIJIJI/KATA

Mimi …….
Ninakiri kwamba Mwanafunzi ……ni mkazi wa Kijiji/Kata ya ……..
SAINI ……
TAREHE ……
MUHURI WA OFISI ……

NB: Fomu hii na fomu ya medical examination zirudishwe shuleni zikiwa zimejazwa kikamilifu siku ya mwanafunzi kuripoti shuleni.

HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI

SHULE YA SEKONDARI ITIGI

Simu: Mkuu wa Shule 0756 658 415/ 0673 988 415 S.L.P. 10,
Makamu M/Shule 0762 624 935/0735 627 770 **ITIGI**

MEDICAL EXAMINATION FORM

Date ……

To the Medical Officer
……..
……..

Dear Sir/ Madam

REF: **REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine Mr. /Miss…… as to his/ her fitness as a full time student of Itigi Secondary School. May I kindly ask you to fill in the particulars given in the form hereunder.

Yours Sincerely

Jacob P. Mwabeza
HEADMASTER

THE HEADMASTER
ITIGI SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 10
ITIGI

TO BE COMPLETED BY THE MEDICAL OFFICER

1. Blood count (White Blood cells)……..
2. Stool examination…….
3. Urine Examination…….
4. Gestation (for girls only)……
5. Veneral disease…….
6. T.B Test…….
7. E.N.T Problems……
8. Defects of (a) The left and right eye…….
   (b) The chest……
9. Any CHRONIC or FAMILY diseases e.g. Epilepsy, Sickle cell etc
   ……..

DECLERATION

I have examined Mr / Miss …….. and certify that he/she is physically fit/ unfit to pursue his/ her studies as stated above.

…….. **……**
Name of Medical Officer **Signature of Medical Officer**

Designation …… **Official Stamp……**